

MKEMIA MKUU AKUTANA NA MKUU WA MKOA WA GEITA



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Meja Jenerali Mstaafu, Ezekiel Kyunga (katikati), akiwa pamoja na Mkemia Mkuu wa Serikali, Prof. Samwel Manyele (kushoto) wakati alipomtembelea ofisini kwake mjini Geita. Kulia ni Meneja wa Kanda ya Ziwa, Bw. Boniventure Masambu. Mkemia Mkuu wa Serikali alijadiliana na Mkuu wa Mkoa wa Geita juu ya hatua ya kufungua dawati la ukaguzi mkoani Geita ili kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi mkoani humo katika uwasilishaji na usafirishaji wa vielelezo vya makosa ya jinai, kuimarisha udhibiti wa matumizi ya kemikali migodini na ukaguzi wa mizigo ya kemikali inayosafirishwa kuelekea nchi za Uganda, Rwanda na Burundi.